UMUHIMU NA MATOKEO YA SALA (MAOMBI)
NIA YA UWEZESHAJI WA SALA.
TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUANGALIA VIFUNGU VYOTE REJEA.

Kwani wafuasi wote wa Yesu, Sala ni ya lazima kama ilivyo kwa mtu kupumua ili aweze kuishi. Hata hivyo katika waraka kwa Waebrania kuna maelezo kuhusu Mungu ambayo ni muhimu kuyatafakari kwanza kabla ya kuanza kufikiria umuhimu wa sala.

Hebu tazama Waebrania kifungu 11 mstari wa 6 na soma kwa uangalifu. Kuna mambo muhimu ambayo hatuna budi kujifunza kutokana na kumbukumbu rejea hii. Kama uakumbuka somo kuhusu imani, utabaini umuhimu wa imani kwa Mungu waliyokuwa nayo Mitume wa Yesu. Hapa tunaambiwa kwamba bila ya imani, haiwezekani kumpendeza Mungu. Aghalabu kwa wale wanaotaka kuwa Mitume, ni sharti waamini kuwa Mungu yupo na kwamba huwapa thawabu ikiwa wanamtafuta.

Je unafikiri ni nini maana ya kumtafuta Mungu ? Je ungefanyaje ili kumtafuta Mungu ? Napendekeza kwamba njia ambayo miongoni mwetu tunaweza kuizingatia ni mifano miwili iliyoonyeshwa katika Matendo ya Mitume. Kwanza chunguza Matendo ya Mitume kifungu 8 mstari wa 27 hadi 30. Kule kuongoka na kubatizwa kwa Muethiopia kulianza kutokana na kununua nakala ya utabiri wa Isaya na kusoma ili ajaribu kuuelewa. Kwa kuwa alidhamiria kumtafuta Mungu katika neno lake, Mungu alimpa msaada aliouhitaji.

Sasa angalia sura ya 10 mstari wa 1 hadi 5. Katika mfano huu Koronelio alikuwa akisali ili apate msaada sala yake ilisikika na mungu ambaye alimwambia atume wahudumu japo kumwuliza mtu ambaye jina lake aliitwa Petro. Mipango ya Petro kusafiri hadi Kaisaria ilitayalishwa ili akamweleze Koronelio kwa undani juu ya habari njema matoke yake Koronelio na familia yake walibatizwa.

Halikadhalika leo, wale wote wanaotaka kumfuata yesu na kutaka kuwa watume wake, unaposali mungu husikia sala zako na atakujibu kwa njia ambayo itakuwa na faida kwako au kwa wale uwapendao Majibu ya sala yako yanawea kuwa kinyume cha matarajio yako, Daima yatakuwa yale Mungu anayolikiri kuwa ni ya manufaa kwako.

Nataka kukuonyesha mifano mingi ambayo sala zilikuwa na matokeo ya kushangaza Hebu tuangaalie kitabu cha kwanza cha Samwel kifungu cha 1 mistari ya 9 hadi 20 kwa vile alikuwa mgumba Hawai bila shaka katika sala yake mara kwa mara alitamka maneno ya kutaka apate mtoto. Hata hivyo, likiwa tukio la maana ya pekee Mungu aliweza kusikia maombi yake na kujibu sala yake. Chunguza maneno ya Hawai "Nimeiacha roho yangu mbele za Bwana"!!.

Hebu angalia Waraka wa Yakobo kifungu cha 5 mstari wa 17 na 18. Hapa Yakobo anasimulia juu ya Sala mbili za Mtume Eliya. Sala ya kwanza inahusu jinsi Mungu atakavyosimamisha mvua na ya pili kwamba mvua ingenyesha tena baada ya kupita miaka mitatu. Unaweza kusoma maelezo kamili katika kitabu cha Wafalme vifungu 17 na 18. Sababu zilizomfanya Mungu akubali sala ya Eliya kwa nguvu zote ni kwa kuwa na watu wa Ufalme wa Kaskazini ya Israel walikuwa wakiabudu sanamu na kudharau maonyo ya Mungu kupitia Manabii wake. Ukame huu mbaya na wa muda mrefu ilikuwa adhabu iliyotumwa kwao.

Katika kitabu cha pili cha Wafalme sura ya 18 hadi 20 tunamkuta Mfalme aliyeitwa Hezekieli. Alikuwa mmoja wa wale wachache waliomwamini Mungu kweli kweli na kuzishika amri zake.

Wafalme wa 2 sura ya 18 mstari wa 6 Wakati Yerusalemu ilipozingirwa na Waasari, Ezekia alisali kuomba msaada kwa Mungu; sura ya 19 mstari wa 15 hadi 19. Majibu ya Mungu yanapatikana katika mistari ya 32 hadi 35. Somo hili peke yake linadhihirisha matokeo Sala na tunaweza kujifunza mengi hata jinsi Ezekia alivyoendelea kumuomba msaada Mungu. Hebu angalia sura ya 20 mistari ya 1 hadi 6. Tunasoma jinsi Ezekia anavyoambiwa na Nabii Isaya kwamba angekufa kutokana na ugonjwa uliokuwa unamsumbua. Jibu la Ezekia ilikuwa ni kumuomba Mungu, mstari wa 3. Mungu anakubali tena mara moja. Isaya alikuwa hajaondoka Ikulu kabla ya Mungu kumuagiza arudi na kumwambia kwamba akamweleze Hezekia kuwa angepewa muda mwingine wa miaka kumi na tano ya kuishi. Pengine ungependa kusoma tena Sura ya 18,19, na 20 ili uweze kujua zaidi maisha ya Elia.

Tumeangalia mifano kutoka katika Agano la Kale na Agano Jipya kuhusu nguvu na matokeo ya Sala; sasa inaatubidi tuangalie maagizo na mfano wa Yesu na Mitume wake.

Sala fupi zilizo nyingi za Yesu kwa Mungu Baba yake tumeandikiwa katika vitabu vya Injili. Mahali pengine tumeambiwa tu kuwa alisali. Ningependa uangalie mfano mmoja wa sala iliyo muhimu ambayo utaipata katika Luka sura ya 6 mstari wa 12. Tunaa

mbiwa na Luka kuwa Yesu alisali kwa Mungu usiku kucha kwa sababu siku ambayo ingefuata ingekuwa muhimu sana. Hana budi kuwachagua Mitume wake kumi na mbili amba watakuwa wafuasi wake wa karibu ili kuendeleza huduma yake. Hakudiriki kufanya kazi hii peke yake bali aliomba msaada. Funzo tunalolipata hapa ni kuwa tunapokabiliwa na maamuzi magumu, tunapaswa kuomba msaada kwa Mungu katika Sala.

Akiwa anatokea chumba cha juu kuelekea Bustani ya Gertheman Yesu alifululiza kusali kwa Baba yake. Tunaweza kusma Sala hii katika Injili ya Yohana sura ya 17. Ningependa uangalie mistari miwili ya 9 na 20. Katika mstari wa 9 Yesu alionyesha kuwa sehemu hii ya Sala yake ilikuwa maalumu kwa Mitume wake na aliwabaini wao kama "Wao ambao nimepewa". Unapkuja katika mstari wa 20 utatambua kuwa Sala hii ilikuwa na mwelekeo wa mambo yajayo na ilijumuisha wale wote ambao watakuwa wanafunzi wa Yesu mpaka kufikia kipindi cha kurudi kwake duniani kama Mfalme. Angalia neno "wao pia niliopewa" inajumuisha wale ambao watakuwa wanafunzi baadaye. Kama unadhamiria kwa dhati kubatizwa kwa jina la Yesu, maneno haya yanakuhusu wewe pia. Kukuita utoke duniani na Mungu kukupa Yesu mwanae. Wazo hili ni la kushangaza na wewe pia unapaswa kuhamasika juu ya jambo hili.

Katika Matayo kifungu cha 6 kutoka mistari ya 9 hadi 13 kuna mfano wa sala ambayo Yesu aliwapa Mitume watarajiwa wote hadi mwisho wa dunia. Inajumuisha mambo yote muhimu ambayo tunapaswa kuuliza na inaanza kwa kuuliza iwapo Ufalme utakuja na kwamba matakwa ya Mungu yatatimizwa duniani. Ukiangalia pia katika mistari ya 14 na 15 utaona kwamba Yesu alifikia mkazo haja ya kusamehe wengine. Tayari alikuwa amekwisha kutoa maagizo mahususi ikijumuisha sala ya mapema katika hotuba hiyo hiyo; sura ya 5 mstari wa 44. Agizo hili la mwisho linaonekana kuwa gumu kulitii lakini lina ujumbe uliotolewa na Yesu kwa moyo wake wa dhati. Unatambua watu wenye tabia maalumu ambao watakuwa watakatifu katika Ufalme ujao katika dunia hii. Iwapo tunaweza kuwaombea waliotukosea na ambao wanaotutesa basi tutakuwa tumeelewa tunachoambiwa na Injili.

Katika orodha ya maagizo yaliyotolewa na Paulo kwa Wathesalonike katika Waraka wake wa kwanza sura ya 5 mstari wa 17, tunayakuta maneno "Sali bila ya ukomo". Mstari wa 18 unaendelea kuagiza, kushukuru kwa lolote. Anaposema kwa lolote, Paulo ana maana sio tu chakula na mavazi, mahali pa kujisetili na upendo kwa wengine lakini pia majukumu yetu ya kila siku ili kuyathibitisha kwa Mungu. Na kujithibitisha kwa Yesu kuwa tu wafuasi wake wa kweli na wa dhati.

Tunapoangalia kwa makini sala aliyofanya Yesu kwa Baba yake katika Bustani ya Gethsemane tunaanza kuelewa hakika ushupavu wake wa kuelewa mpango wa Mungu kumkomboa mwanadamu kutoka katika kifo. Pia tumeanza kuelewa jinsi ushupavu na utiifu wa mapenzi ya Baba yake ulivyokuwa. Tazama Matayo sura ya 26 mistari ya 36 hadi 46. Hizi zilikuwa ni nyakati za huzuni kabla hajakamatwa kushitakiwa hatimaye kifo chake. Sala yake ya kwanza ilikuwa angehurumiwa vitisho na maumivu yaliyokuwa karibu kumpata. Iwapo Sala hiyo ingejibiwa hakika kusingekuwapo kwetu matumaini katika dunia hii. Hata hivyo Sala ya pili inakubali dhabihu ni lazima ifanyike mateso hayana budi kutokea, na maneno yenyewe ni " mapenzi yako yafanyike". Sala ya tatu ikirudia maneno yale yale na kutilia mkazo dhamira ya Yesu kujikabidhi afe kuwa ufumbuzi wa kutisha wa dhambi ya mwanadamu.

Katika Sala hii ya Yesu kwa Baba yake na katika mifano mingine ya sala tuliyoitafakari, tumeona jinsi inavyowezekana kuzungumza na Mungu. Hata hivyo, leo Yesu ni mpatanishi wetu na hii ina maana kwamba anatuombea kwa Mungu. Kwa hiyo, tunaposali hatuna budi kuelekeza sala zetu kupitia kwa Yesu, Injili ya Yohana sura ya 14 mstari wa 12 hadi 14. Mahusiano uliyonayo wewe Mungu na Yesu kupitia Biblia yak yanawezekana kuwa ndiyo jibu la sala zako. Yanawezekana tayari unajua jinsi ya kusali, lakini kama hujui basi tunataraji somo hili fupi litakusaidia.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)